**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Juni, 2023**

**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Mkuu wa Shule: 0757468056/0622824190**

**Makamu Mkuu wa Shule: 0765584518/0685900423**

**Matron: 0766785449/0753860603**

Shule ya Sekondari Mwazye,

S. L. P 02,

**MATAI-KALAMBO**

**Tarehe 13/6/2023.**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ................................**
**……………………………………………..................**
**S.L.P ..........................………………………......**
**……………………………………………..................**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MWAZYE. HALMASHAURI YA KALAMBO MKOA RUKWA MWAKA 2023**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha tano katika Shule hii mwaka 2023. na atasoma tahasusi ya …………

Shule ya Sekondari Mwazye ipo umbali wa Kilometa 60 Kaskazini mwa Manispaa ya Sumbawanga mkoa wa RUKWA. Usafiri wa basi kutoka Manispaa ya sumbawanga unapatikana katika kituo cha mabasi Katumba sumbawanga Nauli ni Shilingi 5000 basi, 25,000 kwa pikipiki na kwa Bajaji 35.000 kwa kukodi.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 14/8/2023 hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 13/8/2023 na Mwisho wa kuripoti ni tarehe 31/08/2023.

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:**

**2.1 Sare za Shule**

**2.2 Wasichana**

i. Sare ya shule hii ni sketi mbili (2) nyeusi Moja na brown Moja
   - Sketi ziwe na marinda kumi na mbili(12)

- Sketi ziwe ndefu zifike kwenye viatu.

ii. Mashati mawili meupe mikono mirefu
iii. Viatu vyeusi jozi mbili vya kamba vyenye soli fupi na visivyochongoka mbele
iv. Soksi jozi mbili nyeupe
v. Sweta la bluu lenye shingo 'v' kwa ajili ya kujikinga na baridi
vi. Tai mbili nyeusi na brown
vii. Rangi ya hijab inayofanana na shati
viii. Shamba dress Moja rangi damu ya Mzee draft kwa ajili ya kushindia
ix. Nywele fupi muda wote hakuna kusuka wala kuweka dawa
x. Sare ya michezo: tracksuit Moja rangi ya blue bahari, t-shirt Moja damu ya mzee,na raba nyeupe jozi moja

**2.3 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:**

i. Madaftari nane quare 3
ii. **Ream (A4)**, Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (HKL,HGL au HGK) na general studies.
iv. Scientific Calculator kwa tahasusi ya HGK na HGL
v. Godoro Moja ft 2 1/2 x 6
vi. Mashuka mawili rangi Blue jozi 1 na Pink jozi 1 blanket 1 chandarura 1 rangi nyeupe
vii. Nguo za ndani za kutosha
viii. Vyombo vya chakula,sahani ,bakuli,kijiko na kikombe
ix. Ndoo 2 ndogo Lita 10 zenye mifuniko
x. Kwanja 1 jembe 1, fagio 2; wa nje (chelewa) 1 na ufagio wa ndani (soft bloom)1

**2.4 Michango Mbalimbali**

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo

ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- ❖ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi.**
- ❖ **Mwanafunzi awapo shuleni, atatakiwa kulala kwenye bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu.**
- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

### 3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;

vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**...................................**

**MWALIMU ESTHER EDWARD MALLYA**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.**

**TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0757468056/0622824190**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0765584518/0685900423**
- **Mwandamizi Taaluma 0765885846**
- **Mwandamizi Malezi 0753442714**